

Mikataba

Karatasi la uhakika wa muongozo wa pesa zako



Mkataba ni nini?

Mkataba ni mapatano ya kisheria. Mapatano ni masikilizano kati ya watu wawili au zaidi.

Unaweza kukubaliana na mkataba kwa kutia sahihi, kwa kusema kwa maneno yako kuwa utafanya hivyo (kwa kusema kwa mdomo) au kwa kutia alama ya kukubali kuwa unakubali kwenye fomu iliyoko kwenye tuvuti.

Kutia sahihi Mkataba

Unakubaliana na mkataba ulioandikwa kwa kuitia sahihi. Hii ni wakati unapoandika jina lako kwenye mkataba (sahihi).

Mkataba kwa maongezi ya mdomo

Unakubaliana na mkataba wa maongezi ya mdomo wakati unapotumia maneno yanayoonyesha kuwa unataka kukinunua kitu au kufanya kitu. hii inahusu maneno kama 'ndio' au 'mimi nakubali'. Kwa kawaida wewe unakuwa na mkataba wa maongezi ya mdomo wakati unapozungumza na mtu kuhusu kupata huduma kama umeme au simu ya mkono. Hii inaweza kuwa kufanyika uso kwa uso au kwenye simu.

Mapatano ni nini?

Mapatano ni maelewano kati ya watu wawili au zaidi. Siyo mkataba. Kwa mfano, kama ukiahidi kumpatia rafiki lifti kwenye gari lako, huu ni mfano wa mapatano. Sio sheria.

Usikubaline na mkataba, isipokuwa wewe unauielewa.

Wewe lazima uelewe kila kitu kabla ya kuingia kwenye mkataba. Kuna mikataba mingi muhimu ambayo wewe unahitaji kutia sahihi. Kwa mfano; kukodisha nyumba, na kufungua akaunti ya benki. Gundua ni wapi unaweza kupata usaidizi kutoka kwa mtu anayeaminika, tena kwa haraka.

Kumbuka

- ▶ Mkataba ni mapatano yenye nguvu za kisheria.
- ▶ Usitie sahihi kwenye mkataba kama wewe hauielewi vizuri.
- ▶ Haiwezekani kufutulia mbali mikataba mingine kwa sababu umebadilisha mawazo

Ni muhimu kuelewa vizuri kabla ya kukubaliana na kitu.

Hayat anamjibu anayebisha mlango na mchuzi anaanza kumueleza kwa haraka kuhusu jinsi ya kununua chombo cha kusafisha nyumba (Vacuum cleaner). Hayat anamruhusu kuingia nyumbani kwake.

Mchuzi anamweleza vile hiyo mashine ya kusafisha nyumba inavyofanya kazi halafu anampatia nakala ya mkataba. Anamweleza Hayat kuwa anahitajika kutia sahihi hati ya mkataba ili kununua ile mashine.

Hayat anonelea vigumu kuuliza maswali kwa sababu mchuzi anaongea haraka na Kingereza bado ni lugha ngumu kwake Hayat. Hayat anamweleza mchuzi kuwa anahitaji usaidizi kuelewa mkataba kabla ya kutia sahihi.

Hayat anamuuliza mchuzi amwachie hati ya mkataba baada ya kumeelezea kuwa anahitaji nafasi ya kuelewa kilichomo ndani yake.

Hayati anamuuliza rafiki yake Miranda usaidizi. Miranda anampeleka Hayat kwenye kituo cha sheria bila malipo ili kumwona mojawapo wa wafanya kazi.

Mfanya kazi anamweleza Hayat kuwa mashine ya kusafisha itamgharimu pesa nyingi sana na ni vizuri kuwa Hayat hakutia sahihi mkataba bila usaidizi. Mfanya kazi anamshauri Hayat kuwa ni muhimu kuuliza usaidizi kwa mtu anayemwamini.



Mahali pa kupata usaidizi na maelezo zaidi

Kwa maelezo zaidi kuhusu mikataba ya mkopo, tembelea tuvuti ya MoneySmart, www.moneysmart.gov.au, au pigia simu 1300 300 630.

Kama una shida na gasi yako, umeme au mkataba wa simu, pigia mtoaji wako wa huduma.

Afisi za haki za kufanya biashara

Kama una shida na wanaochuuza mlango-kwa mlango, gari, simu ya mkono au mkataba wa kukodisha, pigia simu Afisi ya Haki za Kufanya Biashara (Office of Fair Trading) ya Mkoa wako au eneo lako ili ikusaidie wewe.

Ili kupata Afisi ya Haki za Kufanya Biashara (Office of Fair Trading) ya Mkoa au eneo lako, tembelea www.consumerlaw.gov.au

Vituo vya sheria katika Jumuiya

Kama una shida za kisheria na mkataba, wasiliana na kituo cha sheria katika eneo lako bila malipo. Vituo vya sheria katika jumuiya huwa vya kujitawala, vituo hivi hutoa huduma za sheria bila malipo kwa umma. Muungano wa Kimataifa wa Vituo vya Jumuiya vya Sheria (National Association of Community Legal Centres), tembelea tuvuti kwenye www.nacalc.org.au, ni chama cha mkoa pamoja na eneo la jumuiya ya sheria katika Australia. Kwa maelezo kuhusu kituo cha sheria cha jumuiya bila malipo kilicho karibu nawe, tembelea tuvuti kwenye www.nacalc.org.au/directory

Msimamizi wa Idara ya Mawasiliano

Ikiwa wewe unazo shida na mikataba ya simu au tuvuti au mpeanaji huduma, unaweza kutembelea tuvuti ya misimamizi wa idara ya mawasiliano (Telecommunications industry Ombudsman) kwenye www.tio.com.au, au kupiga simu 1800 062 058 - bila malipo ukitumia simu ya nyumbani nchini Australia.